

# Wanyama wanaopatikana kwenye Misitu ya Rubeho na Ukaguru



## Kwa nini mimea na wanyama wa Misitu ya wilaya ya Kilosa na Mpwapwa ni muhimu?

Misitu ya milima ya Rubeho na Ukaguru ni sehemu ya Misitu ya Milima ya Tao la Mashariki. Misitu hii ni muhimu kwa sababu inahifadhi mimea na wanyama aina mbalimbali ambao hawapatikani sehemu nyingine yoyote duniani. Kama Misitu hii itafyekwa viumbe hawa watatoweka. Misitu pia inahifadhi hewa ukaa; inalinda vyanzo vya maji; na pia inatoa madawa ya miti shamba pamoja na mazao mengine ya misitu kwa jamii.

## Tunajuaje kuna wanyama na mimea kwenye misitu hii?

Kupitia mradi wa 'MKUHUMI kwa ajili ya jamii na uhifadhi wa misitu Tanzania' timu ya wataalamu kutoka TFCG na MJUMITA, wakishirikiana na wanajamii, wataalamu wa kienyeji wa miti shamba na wanasayansi, wamekuwa wakijifunza na kujua zaidi kuhusu mimea na wanyama wanaopatikana katika misitu hii. Kwa kutumia mbinu mbalimbali ya kutafiti za kisayansi, waatalamu walibaini aina mbalimbali za wanyama na mimea. Timu hii pia imepiga picha za wanyama na mimea na imechukua baadhi ya sampuli za mimea kwa ajili ya utafiti zaidi.

## Bioanuwai inaingilianaje na MKUHUMI?

Ni muhimu kwamba MKUHUMI unatekelezwa kwa njia ambayo itasaidia kuhifadhi mimea ya asili na wanyama wanaopatikana kwenye misitu ya Tanzania. Jamii inaweza kupata malipo makubwa zaidi kutokana na MKUHUMI kama misitu inaviumbe adimu. Wanyama na mimea yote wanaoonekana kwenye bango hili wanapatikana kwenye ardhi ya vijiji vilivyoko kwenye milima ya Rubeho na Ukaguru na viko ndani ya eneo la utekelezaji wa mradi wa MKUHUMI.



*Nike's squeaker* ni aina ya chura ambaye anaishi kwenye misitu ya Milima ya Rubeho tu. Ni adimu sana na anahitaji misitu iliaweze kuishi.




*Komba wa Mlimani* anapatikana kwenye misitu iliyoko kwenye Milima ya Rubeho. Ni aina adimu na yupo kwenye tishio la kutoweka kutokana na uharibifu wa misitu hii. Anakula wanyama wadogo na gundi itokanayo na miti. Komba huyu hufanya shughuli zake usiku na kulala mchana.



*Nyoka ya msitu wa Uluguru*, anapatikana katika Milima ya Tao la Mashariki pekee. Alipatikana hivi karibuni katika msitu wa Ilole.



*Kanu ya Lowe (Lowe's servaline genet)* anaishi kwenye misitu michache ya Tanzania. Mnyama huyu yuko kwenye tishio la kutoweka kutokana na ufyekaji wa misitu na uwindaji. Ukimuondoa popo, kuna aina tofauti ya wanyama wanyonyeshao wasiyo pungua 31 kwenye misitu hii



*Kinyonga mwenye pembe tatu (Werner's chameleon)* anapatikana kwenye misitu ya milima ya Rubeho na kwenye baadhi ya misitu ya Milima ya Tao la Mashariki. Kuna vinyonga vya aina tofauti visivyopungua aina nne katika Milima ya Rubeho na Ukaguru.



*Minde* ni funo wa msituni ambaye yuko kwenye tishio kubwa kutokana na uwindaji. Anapatikana kwenye misitu michache ikiwemo ya milima ya Rubeho. Kwenye baadhi ya misitu ya Tanzania ambapo walikuwa wanapatikana kwa wingi, kama Tanga, wametoweka kabisa kutokana na uwindaji na uharibifu wa msitu.



*Kwale wa Rubeho* ni aina ya ndege adimu sana ambaye anapatikana kwenye misitu ya Milima ya Rubeho tu na hapatikani sehemu nyingine yoyote duniani. Kwa kuwa wako wachache sana dunia nzima ni muhimu watu wasiwawinde na kuwaua. Pia kuna aina ya ndege wasiopungua 78 katika misitu ya milima ya Rubeho.



*Aina mpya ya Chura*. Aina hii adimu ya chura haijawahi kutambuliwa na wanasayansi wowote mpaka timu ya wataalamu kutoka TFCG na MJUMITA walipotembelea eneo hilo. Chura huyu amegundulika kutoka kwenye eneo la msitu mdogo ujulikanao kama Mikuvi ambao ni sehemu ya msitu wa hifadhi wa Kijiji cha Kisongwe. Ili aina hii ya chura iweze kuishi, ni muhimu kuhakikisha msitu huu unahifadhiwa.